WIZARA YA NISHATI

# NewsBulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 60 | Nov 1 - 30 2024



# MRADI WA UMEME WA RUSUMO WAFIKIA 99%

WIZARA YA NISHATI    +255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**

Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**

Dkt. James Mataragio
Dkt. Khatibu Kazungu

**MHARIRI**

Neema Chalila Mbuja
Prudence Constantine

**WAANDISHI**

Theresa Mhagama
Hafsa Omary
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Immaculate Makilika

**WAPIGA PICHA**

Amanzi Kimonjo
Henry Kilasila
Mustafa Shahame
Isaya Mwakajana

**MSANIFU KURASA**

Brian Mbaga


© NISHATI 2024

# MRADI WA UMEME WA RUSUMO WAFIKIA 99%

- Mawaziri wa Nishati Tanzania Rwanda na Burundi Wajadili Uzinduzi wa Mradi
- Dkt. Biteko Ahimiza Utunzaji wa Mradi na Mazingira
- Asema Utazidi Kuchochea Ukuaji wa Uchumi





Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza katika kikao cha Mawaziri wa kisekta wa nchi wanachama wa Mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo ambao ni Tanzania, Rwanda na Burundi. Kikao hicho kimefanyika leo 15 Novemba.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Nishati wanaosimamia Mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa mawaziri wa nchi za Tanzania, Burundi na Rwanda wamekutana na kujadiliana kuhusu mradi huo ambao upo karibuni kuzinduliwa. " Mradi umefikia asilimia 99.9 na vimebaki vitu vichache ili kuukamikisha, katika kikao cha Baraza la Mawaziri kuhusu mradi tumekubaliana kuwasilisha maombi yetu kwa wakuu wa nchi ili watakapota nafasi mwakani mwezi wa pili waweze kuzindua mradi huu," amesema Dkt. Biteko.

Ameendelea kusema kuwa kwa sasa nchini Tanzania mahitaji ya juu ya umeme ni Megawati 1,800 na kuna uwezo wa kuzalisha Megawati 3,070 hivyo kuna ziada ya umeme.

Amesisitiza " Kuwa na vyanzo vingi ya umeme maana yake tunakuza uchumi wa nchi yetu, asilimia 52 ya umeme wote tunaozalisha unatumiwa na wananchi na asilimia 48 inatumika kwenye viwanda."
Dkt. Biteko ametaja manufaa ya mradi huo kuwa hadi sasa umezalisha ajira kwa watu pamoja na kusaidia uwepo wa miradi mbalimbali kwa ajili ya huduma kwa jamii (CSR) hususan katika Halmashauri ya Ngara. Aidha, mradi huo umeiunganisha Tanzania na nchi za Rwanda na Burundi na pia unatoa fursa ya kuziuzia umeme nchi hizo endapo zitahitaji licha ya uwepo wa megawati 27 zinazopatikana kwa kila nchi.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko ametoa wito kwa jamii kuutunza mradi huo ili uweze kuendelea kutoa umeme " Mradi huu hauwezi kuwa wa kudumu




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko akifungua kikao cha Mawaziri wa kisekta wa nchi wanachama wa Mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo ambao ni Tanzania, Rwanda na Burundi. Kikao hicho kimefanyika leo 15 Novemba

kama hatutunzi mazingira na leo tumetoa maelekezo kwa Baraza tuanze kupanda miti katika eneo la mradi ili kuendelea kutunza mazingira na kuwa na vyanzo vya uhakika vya umeme,"

Imeelezwa kuwa, mradi wa huo wa kufua umeme unaotokana na maji wa Rusumo, umeanza kuzalisha megawati 80 ambazo zinagawanywa kwa usawa wa megawati 27 kwa nchi ya Tanzania, Rwanda na Burundi na hivyo kuzidi kuimarisha gridi za Taifa za umeme.

Mradi huo unaotekelezwa na Kampuni ya Umeme ya Rusumo (RPCL) inayomilikiwa na nchi zote tatu ni kielelezo cha azma ya Serikali ya Tanzania kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika kwa ajili ya shughuli za maendeleo na kijamii.



# TANZANIA KUUNGANA NA DUNIA USALAMA WA AFYA KIMATAIFA

- Dkt. Biteko Ataja Jitihada za Serikali Kuboresha Ajenda ya Mpango wa Kimataifa wa Usalama wa Afya
- Dkt. Biteko Afungua Kongamano la 14 la CUHAS
- Dkt. Biteko Aipongeza CUHAS kwa Tafiti na Mchango wake katika Sekta ya Afya
- Wanasayansi Kuunganisha Afya ya Binadamu, Wanyama na Mazingira kwa Matokeo Bora ya Afya




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza katika ufunguzi wa Kongamano la 14 la Kimataifa la Sayansi la Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Sayansi za Afya (CUHAS) lililofanyika jijini Mwanza lenye kaulimbiu "Afya Moja na Usalama wa Afya wa Kimataifa".

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa mwaka 2015, Tanzania iliunga mkono Ajenda ya Mpango wa Kimataifa wa Usalama wa Afya na kuharakisha utekelezaji wa Sheria za Afya za Kimataifa ili kuzuia magonjwa ya kuambukiza kusambaa kimataifa.
Kupitia tathimini ya pamoja ya mwaka 2023 matokeo ya maendeleo ya Tanzania katika suala hilo inaonyesha hatua kubwa ambapo mwaka 2016 imedhihirika azma imara ya Serikali katika kutekeleza Sheria za Afya za Kimataifa kwa kutumia njia moja ikikubali uunganishaji wa afya ya binadamu, wanyama, na mazingira.

Dkt. Biteko amesema hayo leo Novemba 13, 2024 katika ufunguzi wa Kongamano la 14 la Kimataifa la Sayansi la Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Sayansi za Afya (CUHAS) lililofanyika jijini Mwanza lenye kaulimbiu "Afya Moja na Usalama wa Afya wa Kimataifa".

Ametaja jitihada zilizofanywa na Serikali za kuhuisha miongozo na mipango kazi ili kutekeleza Ajenda ya Mpango wa Kimataifa wa Usalama wa Afya.
"Mwongozo wa Kitaifa wa Maabara na Usalama wa

Bioteknolojia, Ajenda ya Mpango ya Kazi wa Taifa wa Usalama wa Afya, Mpango wa Mkakati wa Afya Moja (2022-2027), Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Usugu wa Vimelea vya Magonjwa dhidi ya Dawa (UVIDA 2023-2028). Pamoja na kuhamasisha ukuzaji na uendelezaji wa raslimali watu na kuchochea ushirikiano wa kisekta," amesema Dkt. Biteko.

Ameendea kusema kuwa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kufanya jitihada za kuhakikisha Usalama wa Afya wa Kimataifa hasa kwa kutoa ufadhili wa masomo na mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa lengo la kuongeza nguvu kazi kila mwaka.

"Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, inathamini mchango wa Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Sayansi za Afya pamoja na Kituo cha Tiba cha Bugando kwa ushirikiano na washirika wa ndani na kimataifa kwa kuwa mabingwa katika nyanja mbalimbali za utafiti zinazohusiana na Usalama wa Afya wa Kimataifa," ameeleza Dkt. Biteko.

Ameongeza "Pia Serikali inathamini mchango uliotolewa na Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Sayansi za Afya kuanzia mwaka 2007 hadi 2023, ambapo kimezalisha zaidi ya wataalamu wa Afya 7,000 katika fani mbalimbali za tiba, dawa, uuguzi, maabara na uchunguzi wa kiafya, na uchomaji wa mionzi ambao wamekuwa mabingwa katika Usalama wa Afya ya Kimataifa."

Aidha, Dkt. Biteko ameipongeza CUHAS kwa kuandaa makongamano hayo ya kisayansi yanayojadili masuala ya kisera ili kutatua changamoto zilizopo katika sekta ya afya na kusema kuwa afya ya binadamu inakumbwa na matishio mengi ili kukabiliana nayo ni lazima kufanya utafiti.

"Nawapongeza kwa kuleta wataalamu kwa ajili ya kujadili masuala ya tiba, niwapongeze pia kwa ugunduzi wa aina ya kirusi kinachoitwa Bugandosis ambacho kimebadilisha mfumo wa tiba na kutoa mchango katika sekta ya afya.

Fauka ya hayo amempongeza Prof. Stephen Mshana kutoka Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Sayansi za Afya kwa kuwa mwanasayansi bora kwa mwaka 2024.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Omary Kipanga amemshukuru Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha sekta ya umma na binafsi hususan katika elimu na afya, akitolea mfano kupitia mradi wa Elimu ya Juu na Mabadiliko ya Uchumi (HEET).

Mradi ambao umesaidia elimu ya juu na kuwezesha ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi ikiwemo kutoa ufadhili wa masomo kwa wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Sayansi za Afya.

Mhe. Kapanga ameongeza kuwa Afya Moja inasisitiza kutafuta suhulu ya pamoja ya changamoto ngumu za kiafya na kuwa Kongamano hilo linasaidia wataalamu, wanasayansi na watunga sera kujadiliana kwa pamoja Usalama wa Afya.

"Ni matumaini yangu tutanufaika kutokana na utaalamu na matokea ya tafiti zilizofanyika awali na mikakati itakayosaidia kupunguza matishio ya afya, nakishukuru Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Sayansi za Afya kwa kuandaa Kongamano hili," amesema Mhe. Kipanga.

Naye, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Sayansi za Afya Bugando (CUHAS), Prof. Erasmus Kamugisha amesema kuwa kauli mbiu ya Kongamano hilo Afya Moja inalenga kuleta muunganiko wa binadamu, wanyama na afya ya mazingira ambayo inaathiri jamii, taifa na dunia katika kufikia matokeo bora ya afya.

Ameongeza kuwa Kongamano hilo linalofanyika kila mwaka limehudhuriwa na takribani washiriki 500 kutoka nchi mbalimbali duniani na litakuwa na tafiti za sayansi 150 zitakazojadiliwa kwa siku mbili.

Inaelezwa kuwa tafiti mbalimbali zinazowasilishwa kupitia makongamano hayo zimeweza kushawishi kubadilishwa kwa miongozo au sera za huduma za afya nchini ikiwemo mabadiliko ya dawa.

Aidha, kwa mwaka 2024 yamechapishwa jumla ya machapisho 271 kuhusu mada mbalimbali za tafiti.

# WANANCHI WACHAGUA VIONGOZI SERIKALI ZA MITAA

- DKT. Biteko apongeza Wananchi Kujitokeza kwa wingi
- Awahimiza kujitokeza kuwachagua viongozi



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, akipiga kura katika kituo cha kupiga kura cha Shule ya Msingi Bulangwa wilayani Bukombe mkoani Geita

Watanzania katika maeneo mbalimbali ya nchi wamejitokeza kupiga kura kwa ajili ya kuwachagua viongozi wao ngazi ya Serikali za Mitaa. Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ametimiza haki yake ya Kikatiba katika Kata ya Bulangwa, Wilayani Bukombe, Geita kisha akawashukuru wananchi kwa kujitokeza kwa wingi kupiga kura. Dkt. Biteko amesema hayo leo Novemba 27, 2024 mara baada ya kupiga kura katika kituo cha kupiga kura cha Shule ya Msingi Bulangwa wilayani Bukombe mkoani Geita. " Zoezi la kupiga kura linaendelea vizuri na wananchi wamejitokeza kwa wingi nawapongeza kwa hilo. Uchaguzi wa mwaka huu umekuwa tofauti kwa sababu ya hamasa kubwa ya kushiriki," amesema Dkt. Biteko. Amesisitiza " Ninaomba watu wote waliojiandikisha watumie haki yao ya kikatiba kwa kujitokeza kwa wingi na kwenda kupiga kura," Kampeni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa zilizinduliwa Novemba 20, 2024 na kuhitimishwa Novemba 26, 2024 baada ya wagonbea kujinadi na kuomba kura kwa wananchi.

# DKT. BITEKO AHIMIZA UPENDO, AMANI NA USHIRIKIANO SENGEREMA

- Asisitiza wananchi kushiriki Uchaguzi Wa Serikali za Mitaa kwa amani
- Asema Sengerema inahitaji maendeleo na si maneno



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akihutubia wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Novemba 1, 2024 eneo la soko la zamani, wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amehimiza upendo, amani na ushirikiano miongoni mwa wananchi wa Sengerema ili waweze kujiletea maendeleo.

Dkt. Biteko ameyasema hayo Novemba 1, 2024 wakati akizungumza katika mkutano wa hadhara katika eneo la soko la zamani, wilayani Sengerema mkoani Mwanza. " Tumekutana hapa kwa kuwa nchi ina amani, watu wa Sengerema tupendane, tushirikiane, tuthaminiane na tujaliane ili tuweze kuwa na fursa ya kujishughulisha na shughuli zitakazotuletea maendeleo," amesema Dkt. Biteko.

Ameongeza " Mhe. Rais amefanya mambo mengi na alipopita hapa alieza, tunapotaja miradi aliyotekeleza tunamtaja

sana yeye Mhe. Rais kwa sababu dhamana ya maendeleo ya Watanzania na wananchi wa hapa Sengerema ipo mikononi mwake,"

Dkt. Biteko ameendelea kwa kusema Sengerema haikuwahi kuwa na hospitali ya wilaya isipokuwa katika kipindi cha Rais Samia imepata hospitali hiyo. Amefafanua zaidi kwa kusema alipoitembelea hospitali hiyo amebaini upungufu wa majengo ambayo ni jengo la upasuaji na kuwa fedha kwa ajili ya ujenzi wake zimeshatolewa tayari, fedha za jengo la wagonjwa mahututi nazo zimefika wilayani hapo na kusema kuwa ujenzi wa uzio wa hospitali utafanyika kwa kutumia mapato ya ndani ya wilaya.

Akizungumzia umeme katika Wilaya ya Sengerema, amesema kuwa vijiji vyote 71 vimepata umeme na kuwa katika vitongoji 425 ni vitongoji vicheche havina umeme na vinafanyiwa kazi ili wilaya hiyo ipate umeme wa uhakika, Dkt. Biteko amesema Serikali inajenga njia nyingine ya umeme kutoka Nyakanazi hadi Igaka na kutoka Igaka hadi Sengerema na kuwa jitihada hizo za Serikali zinatafsiri maendeleo ambayo yanahitajika na watu wa Sengerema na sio maneno pekee.

Aidha, amewapongeza wananchi wa Sengerema kwa kuwa na jitihada katika kuzalisha chakula cha kutosha ambapo wamezalisha zaidi ya tani 500,00 huku mahitaji yakiwa tani 333,000 pekee. Fauka ya hayo, Dkt. Biteko amesema kuwa wananchi wa Sengerema wamempata mbunge mchapakazi Mhe. Hamisi Tabasamu na kumtaka aendeleze juhudi za kuwaletea maendeleo wananchi wake sambamba na kuwahimiza wananchi kuendelea kumpa ushirikiano zaidi mbunge huyo.

Pia, Dkt. Biteko amewaasa wananchi wa Sengerema kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa amani na kufuata taratibu na sheria na kuwa uchaguzi huo usiwe sababu ya kuwagawa.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda amesema kuwa Mkoa wake umejiandaa vizuri kwa ajili ya kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuwa umeshika nafasi ya tatu katika zoezi la kuandikisha wapiga kura kwa idadi kubwa katika Daftari la Wapiga Kura.

Kwa upande wake, Diwani Kata ya Ibisawageni, Mhe. Jumanne Masunga ameipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi mbalimbali ikiwemo kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari katika kata yake. " Hata katika miradi ya maji katika wilaya yetu inaendelea vizuri sasa tumetandaza mabomba kama kilomita 75 ili maji yaweze kuwafikia wananchi wetu. Mwaka jana tumejenga tanki la maji kwa kiasi cha shilingi milioni 554 na tunajenga barabara ya lami, tunaomba utufikishie shukrani zetu kwa Rais Samia na tunamuomba atuongezee bajeti ya ujenzi wa barabara za lami," amesisitiza Bw. Masunga.

# SERIKALI INAENDELEA KUTEKELEZA MRADI WA KUPELEKA UMEME WA GRIDI MTWARA NA LINDI- MHE.KAPINGA

- Lengo ni kuimarisha upatikanaji wa umeme
- Fidia kulipwa kwa wanaopisha mradi



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga Novemba 04,2024 Bungeni jijini DODOMA akijibu swali la Mhe. Zuberi Kuchauka Mbunge wa Jimbo la Liwale, aliyetaka kufahamu uamuzi wa Serikali kuhusu ujenzi wa kituo cha umeme Jimbo la Liwale.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga amesema Serikali inatekeleza mradi wa kuiunganisha Mikoa ya Mtwara na Lindi na umeme wa gridi kutokea Songea kwa kupitia njia ya Tunduru, Masasi -Mahumbika. Mhe. Kapinga ameyasema hayo leo Novemba 04, 2024 bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mhe. Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale aliyetaka kufahamu uamuzi wa Serikali kuhusu ujenzi wa kituo cha umeme Jimbo la Liwale. "Umuhimu wa kujenga kituo cha umeme Liwale upo kwa sababu

kitaboresha upatikanaji wa umeme Liwale, nimhakikishie Mhe. Mbunge kwa sasa tunatekeleza mradi mkubwa wa kupeleka umeme wa gridi ya Taifa kwa mikoa tajwa." Amesema Mhe. Kapinga

Akijibu swali la Mbunge wa Namtumbo, Mhe. Victor Kawawa aliyetaka kufahamu ni lini wananchi waliopisha mradi wa gridi ya Taifa kwenda Mikoa ya Mtwara na Lindi watalipwa fidia, Mhe.Kapinga amesema agizo la Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha wananchi hao wanalipwa fidia linatekelezwa.

Kapinga, ametoa rai kwa wananchi hao kuendelea kutoa ushirikiano kwa kupisha maeneo yao ili mradi uweze kukamilika kwa wakati kwa manufaa ya Taifa.

Akijibu swali la Mbunge wa Meatu, Mhe. Leah Komanya aliyeuliza Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme katika Wilaya ya Meatu, Mhe. Kapinga amesema Wilaya ya Meatu inapata umeme kutokea Kituo cha Kupoza umeme cha Ibadakuli kilichopo Mkoani Shinyanga umbali wa kilomita 135.

Aidha, kukatika kwa umeme wilayani Meatu kunatokana na umbali mrefu wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na uchakavu wa miundombinu ya umeme.

Mhe. Kapinga ameongeza kuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na tatizo hilo ikiwa ni pamoja na kufungwa vidhibiti umeme katika njia ya awali, kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka Mkalama Mkoani Singida hadi Bukundi Wilayani Meatu pamoja na zoezi la kubadilisha nguzo zilizochakaa kwa kuweka nguzo za zege.

"Mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imeanza kutekeleza ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme katika eneo la Imalilo, Wilaya ya Bariadi Mkoani Simiyu ambapo itajengwa line ya umeme kutokea kwenye kituo hicho hadi Meatu." Amesisitiza Mhe.Kapinga.

Akijibu swali la Mbunge wa Bunda Mjini, Mhe. Robert Chacha aliyetaka kufahamu ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa umeme kwenye mitaa ya Halmashauri ya Mji wa Bunda, Mhe. Kapinga amesema tayari Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inatekeleza mradi wa vitongoji kumi na tano.

Akijibu swali la Mbunge wa Tarime Vijijini, Mhe. Mwita Waitara aliyetaka kufahamu ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa umeme katika Jimbo la Tarime Vijijini, Mhe. Kapinga amesema tayari Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inatekeleza mradi wa vitongoji kumi na tano.

Ameongeza kuwa kuanzia mwezi Desemba mwaka huu Serikali itaanza kutekeleza mradi mwingine wa Vitongoji 4,000 nchini.

# KAPINGA ATOA MAAGIZO TANESCO

- Ni kuhusu Vijiji vinavyolipia gharama ya mijini kuunganisha umeme
- Maboresho kituo cha Mbagala kuimarisha upatikanaji umeme Kigamboni, Mbagala na
- Ukanda wa Pwani

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga amesema Serikali inatekeleza mradi wa kuiunganisha Mikoa ya Mtwara na Lindi na umeme wa gridi kutokea Songea kwa kupitia njia ya Tunduru, Masasi -Mahumbika.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo leo Novemba 04, 2024 bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mhe. Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale aliyetaka kufahamu uamuzi wa Serikali kuhusu ujenzi wa kituo cha umeme Jimbo la Liwale.

"Umuhimu wa kujenga kituo cha umeme Liwale upo kwa sababu kitaboresha upatikanaji wa umeme Liwale, nimhakikishie Mhe. Mbunge kwa sasa tunatekeleza mradi mkubwa wa kupeleka umeme wa gridi ya Taifa kwa mikoa tajwa." Amesema Mhe. Kapinga

Akijibu swali la Mbunge wa Namtumbo, Mhe. Victor Kawawa aliyetaka kufahamu ni lini wananchi waliopisha mradi wa gridi ya Taifa kwenda Mikoa ya Mtwara na Lindi watalipwa fidia, Mhe.Kapinga amesema agizo la Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha wananchi hao wanalipwa fidia linatekelezwa.

Kapinga, ametoa rai kwa wananchi hao kuendelea kutoa ushirikiano kwa kupisha maeneo yao ili mradi uweze kukamilika kwa wakati kwa manufaa ya Taifa.

Akijibu swali la Mbunge wa Meatu, Mhe. Leah Komanya aliyeuliza Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme katika Wilaya ya Meatu, Mhe. Kapinga amesema Wilaya ya Meatu inapata umeme kutokea Kituo cha Kupoza umeme cha Ibadakuli kilichopo Mkoani Shinyanga umbali wa kilomita 135.

Aidha, kukatika kwa umeme wilayani Meatu kunatokana na umbali mrefu wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na uchakavu wa miundombinu ya umeme.

Mhe. Kapinga ameongeza kuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na tatizo hilo ikiwa ni pamoja na kufungwa vidhibiti umeme katika njia ya awali, kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka Mkalama Mkoani Singida hadi Bukundi Wilayani Meatu pamoja na zoezi la kubadilisha nguzo zilizochakaa kwa kuweka nguzo za zege.

"Mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imeanza kutekeleza ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme katika eneo la Imalilo, Wilaya ya Bariadi Mkoani Simiyu ambapo itajengwa line ya umeme kutokea kwenye kituo hicho hadi Meatu." Amesisitiza Mhe.Kapinga.

Akijibu swali la Mbunge wa Bunda Mjini, Mhe. Robert Chacha aliyetaka kufahamu ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa umeme kwenye mitaa ya Halmashauri ya Mji wa Bunda, Mhe. Kapinga amesema tayari Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inatekeleza mradi



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga Novemba 04,2024 Bungeni jijini DODOMA akijibu swali la Mhe. Zuberi Kuchauka Mbunge wa Jimbo la Liwale, aliyetaka kufahamu uamuzi wa Serikali kuhusu ujenzi wa kituo cha umeme Jimbo la Liwale.

wa vitongoji kumi na tano.

Akijibu swali la Mbunge wa Tarime Vijijini, Mhe. Mwita Waitara aliyetaka kufahamu ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa umeme katika Jimbo la Tarime Vijijini, Mhe. Kapinga amesema tayari Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inatekeleza mradi wa vitongoji kumi na tano.

Ameongeza kuwa kuanzia mwezi Desemba mwaka huu Serikali itaanza kutekeleza mradi mwingine wa Vitongoji 4,000 nchini.

# TANZANIA KUWA MWENYEJI MKUTANO WA KIMATAIFA WA MATUMIZI BORA YA NISHATI

- Wadau 400 kukutana Arusha
- Kuhusisha majadiliano, kubadilishana uzoefu, fursa za uwekezaji
- Dkt.Doto Biteko kuwa mgeni rasmi
- Ufanisi wa Tanzania Matumizi Bora ya Nishati wapelekea EU kuongeza muda wa ufadhili



Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga akizungumza na Vyombo vya Habari Jijini Dar es Salaam, tarehe 5 Novemba, 2024 kuhusu Mkutano wa Kikanda wa Matumizi bora ya Nishati unaotarajiwa kufanyika Mkoani Arusha mapema mwezi Desemba ukihusisha wadau mbalimbali wa nishati kutoka ndani na nje ya nchi.

Imeelezwa kuwa, Tanzania kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Ubalozi wa Ireland imeandaa Mkutano wa Kikanda kwa nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) unaohusu masuala ya Matumizi Bora ya Nishati.

Hayo yamebainishwa na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga Jijini Dar es Salaam wakati akitoa taarifa kuhusu mkutano huo wa kikanda kwa Waandishi wa habari kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba.

Mhandisi Luoga amesema kuwa, mkutano huo utakaofanyika tarehe 4-5 Desemba 2024, jijini Arusha unatokana na programu ya pamoja ya Serikali ya Tanzania, UNDP, EU na Ubalozi wa Ireland inayohusika na Matumizi Bora ya Nishati iliyoanza kutekelezwa mwaka 2022.

Amesema katika Mkutano huo,



Meneja wa Mradi wa masuala ya Nishati na mabadiliko ya Tabianchi wa Umoja wa Ulaya (EU), Massimiliano Pedretti akifafanua jambo wakati wa mkutano na Vyombo vya Habari Jijini Dar es Salaam, tarehe 5 Novemba, 2024 kuhusu Mkutano wa Kikanda wa Matumizi bora ya Nishati unaotarajiwa kufanyika Mkoni Arusha mapema mwezi Desemba ukihusisha wadau mbalimbali wa nishati kutoka ndani na nje ya nchi.

ujulikanao kama Regional Energy Efficiency Conference (REEC) ambao mgeni rasmi atakuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko unahusisha wadau wa nishati takriban 400 wa ngazi mbalimbali ikiwemo Mawaziri, wataalam na sekta binafsi, utajumuisha kubadilishana uzoefu na uelewa katika masuala ya nishati, fursa zilizopo na uwekezaji.

Akizungumzia pogramu ya Matumizi Bora ya Nishati, Mhandisi Luoga amesema ina umuhimu mkubwa nchini kwani inahusisha matumizi ya umeme kwa ufanisi na kwa ubora, inalenga kupunguza upotevu wa umeme, kupunguza gharama za umeme na kulinda mazingira.

Kuhusu utekelezaji na faida za programu hiyo, Mhandisi Luoga amesema Tanzania tayari imeshaandaa mkakati wa matumizi bora ya nishati wa miaka 10 (2024-2034), kumekuwa na ufadhili wa wanafunzi wa kike katika masuala ya nishati, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limeshaanza kuandaa viwango vya matumizi bora ya nishati kwenye vifaa mbalimbali kama majokofu, pia kuna vijana takriban 152 wamepata ufadhili kutokana na ubunifu katika matumizi bora ya nishati.

Vilevile, Kamishna Luoga ametoa wito kwa Watanzania kutumia vifaa vyenye viwango vya ufanisi bora wa nishati ili kudhibiti upotevu wa umeme na kutumia gharama ndogo katika matumizi ya umeme.

Kwa upande wake, Naibu Balozi wa Ireland nchini, Mags Gaynor amesema Ubalozi huo unafurahishwa na jinsi Tanzania inavyotekeleza Programu ya Matumizi Bora ya Nishati ikiwemo kuandaa mkakati utakaopelekea Tanzania kutekeleza kwa ufanisi zaidi programu husika.

Akizungumzia Mkutano huo wa Kikanda wa Matumizi Bora ya Nishati, amesema ni hatua kubwa katika safari ya mabadiliko kuelekea kwenye matumizi bora ya nishati pamoja na kuwa njia ya kusukuma ajenda ya matumizi bora ya nishati.

Kwa upande wake, Programu Meneja wa Miradi ya Nishati kutoka EU, Massimiliano Pedretti ameipongeza Tanzania kwa utekelezaji wa programu hiyo ambayo imeonesha mafanikio makubwa na kueleza kuwa Umoja huo utaongeza muda wa utekelezaji wa programu hiyo nchini ambayo ilikuwa ikifikia ukomo mwaka huu wa 2024 lakini sasa itaisha mwaka 2025 pamoja na kutanua wigo wa kazi pamoja na ufadhili.

Naye, Abbas Kitogo, Mtaalam wa Miradi kutoka UNDP, amesema Mkutano huo wa kikanda, utakuwa ni sehemu ya kubadilisha ujuzi, uelewa na kuhakikisha kunakuwa na uelekeo mmoja katika matumizi bora ya nishati kwani kila mmoja akifanya juhudi matumizi ya nishati yanatupungua na kuelekezwa kwenye sehemu zenye uhitaji na kupunguza gharama za nishati ambazo zinaweza kuelekezwa kwenye miradi mingine ya maendeleo.

# WIZARA YA NISHATI YAFANYA MAZUNGUMZO NA KAMPUNI YA EQUINOR TANZANIA

- Wazungumzia uendelezaji wa Mradi wa LNG



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt.James Mataragio (tatu kulia) akiongoza kikao kati ya Wizara na Kampuni ya Equinor Tanzania AS. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni Jijini Cape Town wakati wa Mkutano wa Wiki ya Nishati Afrika.

Wizara ya Nishati imekutana na kufanya mazungumzo na Kampuni ya Equinor Tanzania AS kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa Mradi wa Kusindika Gesi Asilia (LNG) pamoja na masuala mengine yanayohusu Gesi Asilia nchini.

Mazungumzo hayo yalifanyika hivi karibuni Jijini Cape Town – Afrika Kusini wakati wa Mkutano wa Wiki ya Nishati Afrika, mkutano ulioleta pamoja wadau zaidi ya 5000 kutoka ndani na nje ya Afrika.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio alisema kuwa Wizara ipo tayari kusikiliza na kuchukua mapendekezo yatakayotolewa na kampuni hiyo yanayolenga kuwezesha utekelezaji wa mradi kwa wakati.

"Niishukuru Equinor Tanzania kwa kuomba kikao hiki muhimu na Wizara. Tunatambua kuwa utekelezaji wa mradi huo wa kusindika gesi asilia unahusisha wadau wengine ambao hawapo hapa ila hiyo haizuii Wizara kukutana na kumsikiliza mdau mmoja mmoja kwani lengo letu ni kuhakikisha mradi huu unatekelezwa kwa ufanisi." alisema Mataragio.

Ujumbe wa Equinor uliongozwa na Makamu wa Rais wa Equinor Kanda ya Bara la Afrika, Bi. Nina Birgitte ambaye pamoja na kueleza masuala ya LNG na kutoa ushauri kwa Wizara, alitumia fursa hiyo kutoa taarifa ya mabadiliko ya uongozi wa juu wa kampuni hiyo nchini Tanzania ambapo alisema nafasi ya Maneja wa Equinor Tanzania ambayo kwa sasa inashikiliwa na Dr. Unni Fjaer itachukuliwa na Bi. Hilde Nafstad kutoka Norway.

Kampuni ya Equinor Tanzania AS ni miongoni mwa wabia wanaohusika katika utekelezaji wa mradi wa LNG nchini Tanzania.

Mradi huo unaolenga kuendeleza gesi asilia iliyogunduliwa katika kina kirefu cha Bahari ya Hindi Kusini mwa Tanzania, unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani takribani Bilioni 42.

Viongozi wengine kutoka Tanzania waliohudhuria kikao hicho ni Kamishna Msaidizi wa Petroli, Mha. Joyce Kisamo, Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Mha. Charles Sangweni na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Bw. Mussa Makame.

# WABIA WA MAENDELEO WAAHIDI KUENDELEA KUSHIRIKIANA NA SERIKALI KUTEKELEZA MIRADI YA REA

- REA YAPONGEZWA KUFIKISHA UMEME VIJIJINI



Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mhe. Fatma Mwassa akizungumza wakati wa Mkutano wa Pili wa Mwaka kati ya Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG) pamoja na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) uliolenga kufanya tathmini ya miradi iliyotekelezwa na wakala huo katika kipindi cha mwaka mmoja.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mhe. Fatma Mwassa ameupongeza Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa kazi kubwa ya kufikisha umeme vijijini ambapo imekuwa ni chachu katika kuboresha huduma za kijamii vijijini pamoja na uchumi wa wananchi.

Mhe. Mwassa ametoa pongezi hizo leo Novemba 8, 2024 Mkoani Kagera wakati akifungua Mkutano wa Pili wa Mwaka kati ya Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG) pamoja na REA uliolenga kufanya tathmini ya miradi iliyotekelezwa na wakala huo katika kipindi cha mwaka mmoja.

“Wakati REA inaanzishwa watu wengi walifikiri ni ndoto ya juu sana. Lakini kwa matokeo ya sasa kila kijiji kina umeme na si ndoto tena. Ni mfano wa kuigwa na kupongezwa. Vijijini sasa tunaona mashine za mazao na viwanda vinafunguliwa na hii inachangia kuimarika kwa uchumi wa wananchi wetu huko vijijini,” amesema Mhe. Mwassa.

Awali Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. Khatib Kazungu amewashukuru Wabia hao wa maendeleo na kuongeza kuwa Serikali itaendelea kushirikiana nao kuendelea kufikisha umeme vijijini ili lengo la kuwafikishia nishati bora wananchi wote, hata walio vijijini, linafikiwa.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. Khatib Kazungu akisisitiza jambo wakati wa Mkutano wa Pili wa Mwaka kati ya Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG) pamoja na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) uliolenga kufanya tathmini ya miradi iliyotekelezwa na wakala huo katika kipindi cha mwaka mmoja.

Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati vijijini (REB), Mhe. Balozi Meja Jenerali (mstaafu), Jacob Kingu amewashukuru Wabia wa Maendeleo kwa mchango wao katika Miradi ya kusambaza nishati vijijini na kuahidi yeye pamoja na Bodi yake kuendelea kuisimamia Menejimenti ya REA kuhakikisha mipango iliyopangwa inafikiwa na fedha zilizotengwa zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG), Morten Heide amesema kuwa wataendelea kushirikiana na Serikali kutekeleza miradi ya kupeleka nishati ya umeme vijijini ili kuendelea kuinua uchumi na kuboresha maisha ya wananchi waishio vijijini.


"Nishati ya umeme ni nishati muhimu sana katika maendeleo ya jamii yoyote duniani. Na sisi kama wabia tunaridhika na jitihada zinazofanywa kusambaza umeme katika vijiji na sasa katika vitongoji. Tunaahidi kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kupeleka umeme vijijini na matumizi ya nishati safi ya kupikia," amesema Heide.

Mkurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini, Mhandisi Hassan Saidy amesema kuwa wakala huo umeweza kufikia mafanikio ya kusambaza umeme vijijini kwa asilimia 99.5, ambapo vijiji 12,240 tayari vimefikiwa na umeme na kuongeza kuwa safari ya kupeleka umeme katika vitongoji imeanza.

"Mafanikio haya makubwa yamewezekana tuu kwa ushirikiano uliopo kati ya serikali yetu na wabia wa maendeleo ambao wamekuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha watanzania, hasa waishio vijijini, wanapata nishati bora ikiwamo nishati ya umeme," amesema Mhandisi Saidy.



Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG), Morten Heide akizungumza wakati wa Mkutano wa Pili wa Mwaka kati ya Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG) pamoja na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) uliolenga kufanya tathmini ya miradi iliyotekelezwa na wakala huo katika kipindi cha mwaka mmoja.




Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mhe. Fatma Mwassa akiwa kwenye picha ya pamoja na Wabia wa Maendeleo katika Sekta ya Nishati (EDPG) pamoja na viongozi mbalimbali wa Serikali na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) mara baada ya Mkutano wa Pili wa Mwaka kati Wabia hao na REA uliolenga kufanya tathmini ya miradi iliyotekelezwa na wakala huo katika kipindi cha mwaka mmoja.

# MITUNGI YA GESI YA KUPIKIA 9,765 KUSAMBAZWA RUKWA



Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Mhe. Makongoro Nyerere akizungumza na Mkurugenzi wa Teknolojia za Nishati Jadidifu na Mbadala kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Advera Mwijage pamoja na Afisa kutoka REA, Salum Kazukamwe walipofika ofisini kwake kwa ajili ya kutambulisha kampuni iliyoshinda kusambaza na kuuza kwa bei ya ruzuku mitungi ya gesi ya kilo sita pamoja na vifaa vyake katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji katika Mkoa huo.

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Mhe. Makongoro Nyerere amewataka Watanzania kuendelea kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhamasisha na kuchochea ajenda ya nishati safi ya kupikia nchini.

Hayo yamebainishwa leo Novemba 21, 2024 na Mhe. Nyerere mara baada ya uwasilishwaji wa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya REA iliyowasilishwa na Mkurugenzi wa Teknolojia za Nishati Jadidifu na Mbadala, Mha. Advera Mwijage.

Amesema, Rais Samia anaendelea kuipeleka ajenda ya nishati safi kimataifa ili kuhakikisha watu wanapika katika mazingira salama kiafya na kimazingira.

Mhe. Nyerere ameongeza kuwa, suala la Nishati Safi ya Kupikia sasa ni ajenda ya kimataifa na wataibeba katika kuelimisha umma kuhusu matumizi salama ya nishati hiyo kwa upana.

Kwa upande wake, Mha. Mwijage amesema lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapika katika mazingira salama na kwamba hatua hiyo itawezekana kwa kupatikana kwa nishati safi ya kupikia iliyo nafuu inayopatikana na kutumika kwa urahisi.

Ameongeza kuwa, mtoa huduma kampuni ya Taifa Gas Limited atahudumia wilaya zilizopo ndani ya Mkoa wa Rukwa kwa kusambaza mitungi 9,765 kwa bei ya ruzuku mitungi ya gesi ya kilo sita pamoja na vifaa vyake katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji.

Amezitaja wilaya zitakazonufaika kuwa ni pamoja na Wilaya ya Kalambo, Sumbawanga na Nkasi.

# ZAIDI YA BILIONI 11 KUSAMBAZA UMEME VITONGOJINI SHINYANGA

- Kunufaisha Kaya 2,970 katika Vitongoji 90 ndani ya Wilaya Tatu
- RC Macha asema Umeme ni kipaumbele cha Rais Samia




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Anamringi Macha akizungumza wakati wa kutambulishwa Mkandarasi aliyeshinda zabuni ya kutekeleza mradi wa Shilingi Bilioni 11.18 wa kusambaza umeme katika vitongoji 90 utakaonufaisha Kaya 2,970 Mkoani Shinyanga.

Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inatekeleza mradi wa Shilingi Bilioni 11.18 wa kusambaza umeme katika vitongoji 90 utakaonufaisha Kaya 2,970 Mkoani Shinyanga.

Msimamizi wa Miradi ya REA Kanda ya Magharibi, Mhandisi Robert Dulle amebainisha hayo Novemba 05, 2024 Mkoani Shinyanga mbele ya Mkuu wa Mkoa huo, Mhe. Anamringi Macha wakati wa kumtambulisha Mkandarasi aliyeshinda zabuni ya kutekeleza mradi huo Kampuni ya wazawa ya Derm Group (T) Limited ya Jijini Dar es Salaam.

"Tunamshukuru Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kiasi cha shilingi 11,184,759,397.2 kitumike kusambaza umeme katika vitongoji 90 Mkoani hapa, leo hii tumefika hapa kumtambulisha Mkandarasi na tayari maandalizi ya awali ya kutekeleza mradi yameanza," alisema Mhandisi Dulle.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mhe. Anamringi Macha aliipongeza REA kwa kutekeleza majukumu yake kwa uwazi na kwa utaratibu iliyojiwekea wa kutambulisha wakandarasi kwa viongozi wa Mkoa na Wilaya kote nchini.

"Ujio wenu hapa ni habari njema sana kwa mustakabali mzima wa maendeleo ya Mkoa wetu; pamoja na huduma zingine za jamii huduma ya umeme imepewa kipaumbele kikubwa na Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, umeme

ni injini ya uchumi hili halina ubishi na sasa matumizi ya umeme yameongezeka, mahitaji kwa ajii ya majumbani na pia kiuchumi," alisema Mhe. Macha

Alisema Mkoa wa Shinyanga unaendelea kukua kwa kasi na kwamba kwa sasa shughuli za kiuchumi zimeongezeka ikiwemo uwepo wa viwanda vidogo na vikubwa ambavyo vyote vinahitaji umeme.

"Hapa Shinyanga mbali na madini pia tunashughulika na kilimo cha mpunga na tungependa kuona mkulima akiongeza thamani ya mazao yake hukohuko unapozalishwa mpunga kwa kukoboa na kupata mchele na hapa faida itaongezeka sambamba na kuandaa ajira na fursa zingine vijijini," alisema.

Aidha, alimtaka Mkandarasi kuhakikisha anatekeleza mradi kwa ubora na anakamilisha kwa wakati kwani tayari miundombinu ipo hivyo hakuna changamoto yoyote itakayokwamisha utekelezaji wa mradi.

"Tunafuraha kuona zipo kampuni za kitanzania zenye uwezo wa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo hii ya umeme ikiwemo kampuni hii ya Derm, tunatoa wito pia kutumia huduma na watoa huduma kwenye maeneo ya mradi, tutoe kipaumbele kwenye kazi zisizohitaji ujuzi mkubwa kwa wananchi wa maeneo ya mradi," alisema.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi wa kufikisha umeme katika vitongoji Mkoani humo, Mhandisi Dulle alisema Kati ya vitongoji 2,703 vilivyopo mkoani humo, vitongoji 930 vimefikishiwa umeme na kwamba vitongoji 90 vitakavyopata umeme awamu hii vitaongeza idadi ya vitongoji vitakavyokuwa na umeme Mkoani Shinyanga.

Alisema mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miezi 24 ambapo utekelezwaji wa mradi ulianza tarehe 3 Septemba, 2024 na utakamilika ifikapo tarehe 19 Agosti 2026 na kwamba vitongoji vitakavyobaki vitaendelea kusambaziwa umeme kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mhandisi Dulle alibainisha kuwa mradi unatekelezwa katika majimbo sita kutoka katika Wilaya za Shinyanga, Kahama na Kishapu na kwamba kila jimbo vitongoji 15 vitanufaika.

"Mradi huu unalenga kupeleka umeme katika majimbo ya Shinyanga, Solwa, Kishapu, Msalala, Ushetu na Kahama," alisema Mhandisi Dulle.

Aidha, Mhadisi Dulle aliainisha hali ya upatikanaji wa umeme maeneo ya vijijini Mkoani humo sambamba na miradi iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa ambapo alisema Kati ya vijiji 506 vilivyopo mkoani humo, vijiji 485 vimefikishiwa umeme ambayo ni sawa na asilimia 96 na kwamba vijiji 21 vilivyobaki vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa pili (REA3R2) chini ya Mkandarasi Tontan Project Technology LTD JV Group Six International.

Alisema vijiji hivyo vipo katika Wilaya ya Kahama na kwamba Mkandarasi anatarajiwa kukamilisha hivi karibuni.

# RAIS SAMIA APELEKA NEEMA TABORA

- AIDHINISHA BILIONI 19 KUSAMBAZA UMEME VITONGOJINI
- KAYA 5,940 KUTOKA KATIKA VITONGOJI 180 KUNUFAIKA REA-TABORA




Msimamizi wa Miradi ya REA Kanda ya Magharibi, Mhandisi Robert Dulle akizungumza mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha (hayupo pichani) Novemba 7, 2024 wakati wa kumtambulisha Mkandarasi anayetekeleza mradi wa kusambaza umeme vitongojini Tabora Kampuni ya Sinotec Company Ltd kutoka nchini China

Wakala wa Nishati Vijijini (REA) unatekeleza mradi wa Shilingi Bilioni 19 wa kusambaza umeme katika vitongoji 180 utakaonufaisha Kaya 5,940 Mkoani Tabora.

Hayo yameelezwa na Msimamizi wa Miradi ya REA Kanda ya Magharibi, Mhandisi Robert Dulle Novemba 07, 2024 Mkoani Tabora mbele ya Mkuu wa Mkoa huo, Mhe. Paul Chacha wakati wa kumtambulisha Mkandarasi aliyeshinda zabuni ya kutekeleza mradi huo Kampuni ya Sinotec Company Ltd kutoka nchini China.

"Napenda kuwafahamisha wananchi wa Tabora kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta. Samia Suluhu Hassan ameridhia kiasi cha shilingi 19,057,015,682.55 kitumike kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vitongoji 180 mkoani hapa na leo hii tupo hapa kumtambulisha mkandarasi anayetekeleza mradi huu," alibainisha Mhandisi Dulle.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mhe. Paul Chacha alimuelekeza Mkandarasi kuhakikisha anakamalisha kazi hiyo kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa na aliipongeza REA kwa kuendelea kutimiza dhamira ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa vitendo.

Akielezea utekelezaji wa mradi, Mhandisi Dulle amesema unatekelezwa ndani ya majimbo yote 12 ya mkoani humo na kwamba unatekelezwa kwa muda wa miaka miwili na utakamilika Mwezi Agosti, 2026 ambapo kila jimbo vitongoji 15 vitanufaika.

Amefafanua kuwa hadi sasa vitongoji vilivyosambaziwa umeme ni vitongoji 1,323 kati ya vitongoji 3,749 na kwamba vitongoji vvitakavyosalia vitasambaziwa umeme kulingana na upatikanaji wa fedha.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha akitoa maelekezo kwa Mkandarasi Kampuni ya Sinotec Company Ltd kutoka nchini China (hayupo pichani) wakati alipotembelewa na Maofisa kutoka REA kwa ajili ya kumtambulisha mkandarasi huyo ambaye ameshinda zabuni ya kusambaza umeme katika vitongoji 180 mkoani humo Novemba 7, 2024




Meneja wa Mradi wa kusambaza umeme kwenye vitongoji 180 Mkoani Tabora kutoka Kampuni ya Sinotec Company Ltd ya China, Mhandisi Alphred Kessy akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kutambulishwa na REA kwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora Paul Chacha (hayupo pichani), Novemba 7, 2024. Wengine katika picha ni viongozi kutoka kampuni hiyo.

Mhandisi Dulle amesema Mradi umelenga kusogeza miundombinu ya umeme kwa wananchi katika majimbo yote ili waweze kunufaika na nishati ya umeme katika kujiletea maendeleo hasa katika kuongeza thamani ya mazao, ufundi seremala, viwanda vidogo vidogo, mashine za kusaga na kukoboa sambamba na shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii.

"Vitongoji vitakavyonufaika ni kutoka katika Majimbo ya Sikonge, Urambo, Igalula, Tabora Kaskazini, kaliua, Ulyankulu, Bukene, Nzega Vijijini, Nzega Mjini, Igunga, Tabora Mjini na Manonga ambapo kila jimbo litapata vitongoji 15, Mashine umba 15 na wateja 495 na msongo mdogo (LV) umbali wa kilomita 30," amefafanua Mhandisi Dulle.

Amesisitiza kuwa gharama ya kuunganishiwa umeme kwa wananchi ndani ya vitongoji hivyo ni shilingi 27,000 na kwamba mradi hautakuwa na fidia.

Mhandisi Dulle amesisitiza kuwa Wakala kwa kushirikiana na TANESCO unaendelea kutekeleza miradi mbalimbali nchi nzima pamoja na kuwasimamia kwa karibu wakandarasi wote waliopewa zabuni ya kutekeleza miradi na kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kwa ubora uliopangwa ili iweze kuwanufaisha wananchi kama ilivyo dhamira ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Naye Meneja wa Mradi kutoka Kampuni ya Sinotec Company Ltd, Mhandisi Alphred Kessy alimuhakikishia Mkuu wa Mkoa kuwa watakamilisha mradi kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.


For more info
www.nishati.go.tz
The United Republic of Tanzania
Ministry of Energy